

Athari ya Maneno ya Mkopo ya Kiingereza katika Fonolojia ya Kihehe

*Ernest Daimon Haonga
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere*

Ikisiri

Makala hii inachunguza athari za maneno ya mkopo ya Kiingereza katika fonolojia ya Kihehe. Fonolojia ya Kihehe inaonesha ongezeko la idadi ya fonimu na miundo ya silabi tangu ilipoanza kupokea maneno ya mkopo kutoka lugha mbalimbali za kigeni ikiwemo Kiingereza. Utafiti huu unatumia ushahidi wa maneno 84 ya mkopo ya Kiingereza yaliyokusanywa kwa kusikiliza masimulizi, usomaji matini na majadiliano kubainisha athari yake katika fonolojia ya Kihehe. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data uliongozwa na nadharia ya usilimisho iliyopendekezwa na Jean Piaget. Matokeo ya utafiti yanaonesha fonolojia ya Kihehe imeathiriwa na uhamishaji na usilimishaji wa moja kwa moja wa maneno ya mkopo ya Kiingereza. Athari kubwa ni kuwepo kwa fonimu konsonanti saba, sauti ng'ong'o nne na miundo nane ya silabi za mkopo katika lugha ya Kihehe. Tumebaini usilimishaji na uhamishaji ni michakato inayochagiza mabadiliko ya orodha ya fonimu za Kihehe. Hivyo maneno ya mkopo ya Kiingereza yanaimarisha lugha ya Kihehe kwa kujaza mapengo ya kiisimu, kileksika na maana yanayosababishwa na tofauti za kitamaduni na kiteknolojia.

Maneno Muhimu: Maneno ya Mkopo, Usilimishaji, Uhamishaji, Irabu-Unganifu.

Utangulizi

Maneno ya mkopo ni vipashio vya kiisimu vinavyokopwa na lugha moja kutoka lugha nyingine kama matokeo ya makutano ya lugha katika muktadha wa mawasiliano. Maneno hayo huingia katika lugha fulani pale wazungumzaji wanapoanza kutumia maneno ya mkopo sambamba na maneno mengine katika lugha yao kwa kubadili msimbo. Kadri mchakato wa ubadilishaji msimbo unavyoendelea kwa muda mrefu, wasemaji huanza taratibu kuunganisha na kutumia maneno ya mkopo kama maneno asilia ya lugha yao (Dworkin, 2012). Hivyo, kubadilisha msimbo ni sharti muhimu la lugha kuingiza maneno ya mkopo na vipengele vingine vya kiisimu.

Ingawa mchakato wa ukopaji hutokea ili kujaza mapengo ya kileksika yanayosababishwa na ukosefu wa baadhi ya sauti, leksimu na maana mahsusni katika lugha pokezi, wakati mwingine huhusisha maneno ambayo maana zake tayari zipo katika lugha pokezi (Campbell, 1998). Hivyo kuna ukopaji unaochagizwa na kukosekana kwa kisawe chenye maana fulani katika lugha na ukopaji unaotokana na utamaduni au nyongeza tu ya kisawe hata kama lugha husika ina kisawe chenye maana sawa na kinachokopwa. Haspelmath (2009) anaeleza kuwa, neno la mkopo katika lugha pokezi haliingii moja kwa moja katika mfumo wa mawasilino kwa sababu lina sifa za kifonolojia ambazo mara nyingi hazitamkiki kwa wazungumzaji wa lugha inayopokea. Ili neno la mkopo likubalike, lazima lihusishwe na fonolojia ya lugha pokezi na au liingizwe kama lilivyo pamoja na sifa zake za kifonolojia (Andersson, Sayeed na Vaux, 2015; Coetsem, 2016). Lugha ya Kihehe ni moja ya lugha zilizopitia mifanyiko hiyo ili kuwezesha baadhi ya sauti na leksimu za mkopo kutumika na wazungumzaji wake jambo lililosababisha athari za kifonolojia katika Kihehe zinazobainishwa na makala hii.

Lugha ya Kihehe

Kihehe ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa sehemu za Kaskazini na Mashariki katika nyanda za juu Kusini mwa Tanzania. Kuligana na uainishaji wa Guthrie (1948), Kihehe kinapatikana katika kundi G60 la lugha za Kibantu. Katika kundi hilo, Kihehe kimepewa namba G62. Idadi ya wasemaji wa Kihehe inakadirisha kuwa 1,425,000 (Ethnologue, 2020). Kihehe kinatajwa kuwa mojawapo ya lugha kubwa za kijamii nchini Tanzania; nyingine zikiwa ni Kisukuma, Kinyamwezi, Kihaya,

Kimakonde na Kinyakyusa (LoT, 2012). Kihehe kinatumika katika shughuli za kawaida za jamii ya Wahehe kutokana na miongozo ya matumizi ya lugha nchini Tanzania. Kimsingi udhibiti wa matumizi ya lugha za jamii za kikabila katika Nyanja rasmi, umechagiza lugha ya Kihehe kupokea maneno ya mkopo kutoka Kiingereza.

Hali ya Makutano ya Kihehe na Kiingereza

Makutano kati ya Wahehe na Waingereza yalianza mwaka 1850 wakati Wamisionari wa Ulaya walipoanza kueneza Ukristo Tanganyika. Makutano yaliongezeka zaidi miaka ya 1940 wakati Tanganyika ilipokuwa koloni la Waingereza. Kipindi hiki Kiingereza kilitumika chombo cha mawasiliano serikalini. Pia Kiingereza kilifundishwa kama somo la lazima darasa la tatu, na lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na elimu ya juu (Blommaert, 2013). Kutokana na dhima hizo, Kiingereza kiliendelea kufahamika zaidi na watu wa makabila mbalimbali wakiwamo Wahehe kutokana na matumizi yake katika sekta rasmi (Batibo, 1996 na Swilla, 2000). Hivi sasa lugha ya Kiingereza imekuwa na ushawishi mkubwa katika lugha za kikabila nchini Tanzania kutokana na ukweli kwamba inapewa daraja la juu la kijamii na kiuchumi kiasi kwamba watu wanaihusisha na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Sambamba na hayo, ni wazi kuwa, lugha ya Kiingereza imekuwa chanzo chenye mvuto zaidi wa viambajengo vyta kileksika kwa lugha mbalimbali za dunia kutokana na kutawala kwake. Kihehe ni mojawapo ya lugha za ulimwengu ambazo zimeathiriwa na Kiingereza kwa kukopa vipengele vyta kisimu. Ushawishi wa Kiingereza katika lugha zingine unatokana na lugha hiyo kuzungumzwa na watu wengi na kuwa lugha ya sayansi na teknolojia katika jumuiya ya kimataifa. Crystal (2003) anaeleza kuwa Kiingereza kimekuwa lugha ya kwanza katika sehemu mbalimbali za dunia, lugha ya pili muhimu kwa baadhi ya Waasia na Waafrika na chombo muhimu cha mawasiliano ya kimataifa. Katika muktagha wa mawasiliano lugha ya watu wanaotawala huathiri lugha ya watu walio chini ya utawala katika hali ya kukutana. Kwa hiyo, kwa kuwa Kihehe ni lugha ya hadhi ya chini kuliko Kiingereza, kinakuwa katika mwelekeo wa kuathiriwa na mchakato wa kukopa katika makutano yoyote kati yake.

Maandiko Kuhusiana na Ukopaji wa Kifonolojia

Maandiko yanaonesha lugha zote zinapokuwa katika makutano huathiriana kwa namna mbalimbali. Ukubwa wa athari za maneno ya mkopo kwenye fonolojia ya lugha pokezi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine (Thomason, 2001). Athari hizo zinabainika katika lugha ikiwa utafanyika uchunguzi wa lugha kisinkronia na kidaikronia. Mathalani kuna ushahidi kwamba, Kiingereza cha zamani kilikuwa hakina konsonanti /f/, /θ/ na /s/, lakini makutano yake na Kifaransa yaliibua konsonanti /v/, /ð/ na /z/ zilizobainishwa kwenye maneno ya mkopo kama vile wife / wives, bath / bathe na house / house (Andersson, Sayeed na Vaux, 2015).

Smith (2007) anabainisha kuwa, ingawa kanuni za kifonotakitiki za Mame-Hawai hazikuruhusu koda na vianzio changamano kwa sababu muundo wa silabi zake ulikuwa ni K(I), Kihawai cha sasa kinaruhusu koda; sababu ya makutano ya muda mrefu na Kiingereza. Andersson, Sayeed na Vaux (2015) wanaeleza kwamba, katika Kihawai, konsonanti za kigeni kutoka Kiingereza hubadilishwa na konsonanti asilia ambapo / b/ na /f/ hubadilika kuwa /p/; /v/ hubadilika na kuwa /w/; /r/ inabadilika kuwa /l/; /ŋ/ inabadilika kuwa /n/; na fonimu /t, d, θ, s, z, ð/ na ðz zinaungana na kuwa fonimu /k/. Usilimishaji na uhamishaji huo wa sauti za mkopo inaelezwa kuwa huchochewa zaidi na kuwepo kwa idadi ndogo ya konsonanti katika orodha ya fonimu za Kihawai.

Pia Sitali-Mubanga (2018) anabainisha kuwa maneno ya mkopo ya Kiingereza yanaathiri fonolojia ya neno la Ki-Silozi kuititia usilimishaji wa irabu na konsonanti za mkopo. Mchakato huo unahuishisha urekebishaji wa irabu za mkopo kama vile /a/, /ɔ:/, /e/, /i/, /ea/, /ɜ:/, na /ee/ /i:/, na pia konsonati /c/[k], /c/[s], /b/, /f/[ch], /g/, na /ch/ [k]. Wazungumzaji wa Ki-Silozi hurekebisha irabu na konsonanti za mkopo ili ziendane na fonolojia yake kuititia ama upachikaji, udondoshaji, ubadilishaji wa vipengele na metathesis. Wakati waandishi wakikubaliana kuwapo kwa athari za kiisimu katika lugha pokezi kutokana na maneno ya mkopo, bado hakuna taarifa za wazi zinazoonesha namna maneno ya mkopo

ya Kiingereza yalivyoathiri fonolojia ya Kihehe. Hivyo basi, kuna pengo la maarifa katika kipengele hicho linaloshughulikiwa na mada hii.

Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya usilimisho iliyopendekezwa na Jean Piaget mwaka 1950 ilitumiwa kuchunguza athari za maneno ya mkopo katika fonolojia ya Kihehe. Katika mada hii, dhana ya usilimisho inahusiana na urejeshi na uendelevu kubaini mabadiliko yanayotokea katika fonolojia ya Kihehe kutokana na uingizaji wa maneno ya mkopo. Katika fonolojia, usilimisho ni nadharia ambayo kwayo sauti hufanana zaidi na sauti zilizo karibu ndani ya neno au katikati ya maneno (Cherry, 2018). Nadharia ya usilimisho ilitumika kurejelea michakato ya kidaikroniki na kisinkroniki. Mchakato wa kidaikroniki ulilenga kubaini ukopaji ambaao ulifanyika zamani wa sauti ambazo hazikuwepo katika Kihehe kama vile /r/, /z/, /ʃ/, /dʒ/, /ndʒ/, na /ð/; na mchakato wa kisinkroniki unarejelea hali ya sasa ambapo wazungumzaji hupokea maneno ya mkopo ambayo yana sauti zilizotajwa bila kusilimisha.

Nyenko na Mbinu

Data za msingi zilikusanya katika mji wa Kilolo na Kalenga mkoani Iringa, kwa kusikiliza masimulizi na mijadala katika vikundi lengwa. Data zilikusanya katika mazungumzo ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watoataarifa katika sehemu tofauti kinapotumika Kihehe, hususani katika sherehe za mazishi, mashamba ya nyanya, kwenye vituo vya mabasi, madukani, sokoni na karakana. Data iliyokusanya kwa njia ya usaili wa mdomo ilihuisha watoataarifa 36. Data iliyokusanya kwa njia ya masimulizi, ilihakikiwa uthabiti wake kupitia majadiliano na vikundi lengwa. Uteuzi wa watoataarifa ulifanywa kimakusudi kwa kuzingatia kuwa ni wazungumzaji wazawa wa Kihehe. Michakato hiyo kwa pamoja ilivezesha kupatikana kwa maneno ya mkopo ya Kiingereza 84 katika lugha ya Kihehe. Data hiyo iliyokusanya ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa maelezo.

Matokeo ya Uchunguzi wa Athari za Kifonolojia za Maneno ya Mkopo

Sehemu hii, inawasilisha uchambuzi na mjadala wa kiisimu kuhusu athari za maneno ya mkopo ya Kiingereza katika fonolojia ya Kihehe. Hata hivyo, kabla ya uchambuzi, tunabainisha kwa muhtasari vipengele vya kifonolojia vya Kihehe na Kiingereza ili kuweza kutambua kwa urahisi vipengele vilivyoamishwa kutoka Kiingereza kwenda Kihehe.

Mfumo wa Fonimu za Kihehe

Fonimu ni kipashio cha kifonolojia chenye uaminifu wa kubainisha maana ya neno. Kihehe kina fonimu ishirini na nane, ambapo konsonanti ni kumi na nane na irabu kumi. Konsonanti hizo na sifa zake bainifu zimeoneshwa katika Jedwali Na 1.

Jedwali Na. 1: Fonimu Konsonanti za Kihehe

Mahali pa Matamshi ➔		Midomo	Midomo-meno	Ufizi	Gumu	Kaaka	Kaaka laini	Glota
◀ Namma ya Utankaji	Vipasuo	Sighuna	p	t		k		
	Ghuna	b		d		g		
	Vikwamizi	sighuna	f	s			h	
	Ghuna		v					
	Vipasuo-kwamizi	sighuna			ʃ			
	Kitambaza	Ghuna		l				
	Nazali	Ghuna	m	n	p	ŋ		
	Viyeyusho	Ghuna	w			j		

Chanzo: Haonga (2013)

Jedwali linaonesha kuwa konsonanti za Kihehe zinakaribiana sana kati ya hati za kifonetiki na hati za kawaida (otograafia). Zipo konsonanti tano tu ambazo unukuzi wake wa kifonetiki unatofautiana na hati za kawaida. Fonimu konsonanti hizo zimebainishwa katika mfano (2).

(1) Herufi za Kifonetiki

[j]	y	mfano <i>yeeki</i> , “for what”
[t]	ch	<i>chaana</i> ‘kid’
[n]	ng’	<i>ng’ingo</i> ‘skin’
[n]	ny	<i>nyuulo</i> ‘wild forest’
[nn]	ng	<i>ngoolo</i> ‘shout’

Kiingereza kina fonimu arobaini na nne; konsonanti ishirini na nne na irabu ishirini. Kati ya konsonanti hizo vipasuo ni sita /p/, /b/, /t/, /d/, /k/ na /g/; vikwamizi tisa /f/, /v/, /θ/, /ð/, /s/, /z/, /ʃ/, /ʒ/ na /h/; vizuiokwamizi viwili /ʃ/ na /dʒ/; nazali tatu /m/, /n/ na /ŋ/; kitambaza kimoja /l/; na viyeyusho viatu /w/, /r/ na /j/ (Roach, 2000). Jedwali Na 2 linaonyesha orodha ya konsonanti za Kiingereza.

Jedwali Na. 2: Fonimu Konsonanti za Kiingereza

	Midomo	Midomo Meno	Ufizi Meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	Glota
Vipasuo	p b			t d		k g	
Nazali	m			n		ŋ	
Vikwamizi		f v	θ ð	s z	ʃ ʒ		h
Kipigo				r			
Vizuiokwamizi					tʃ dʒ		
Viyeyusho	w					j	
Kitambaza				l			

Chanzo: Roach (2000)

Tofauti moja ya wazi inayobainika katika majedwali hayo ya konsonanti za Kihehe na Kiingereza ni idadi ya konsonanti zinazopatikana ndani yake. Mathalani tumebainisha kuwa Kihehe kina idadi ya Konsonanti 18 wakati Kiingereza kikiwa na konsonanti 24. Uchunguzi unaonyesha karibia konsonanti zote za Kihehe na Kiingereza zinatamkiwa mahali pa mamtamshi panapofanana isipokuwa konsonanti chache. Wakati orodha ya konsonanti za Kiingereza ina kimadende kimoja /r/, orodha ya Kihehe haina sauti hiyo. Kiingereza kina vikwamizi vitano /θ/, /ð/, /z/, /ʃ/ na /ʒ/ na hivyo kufanya idadi ya vikwamizi kuwa tisa, wakati Kihehe kina vikwamizi vinne /f/, /v/, /s/ na /h/. Pia, Kiingereza kina vizuiokwamizi viwili /dʒ/ na /ʃ/ ilhali Kihehe kinacho kimoja tu /ʃ/. Pia Kiingereza kina konsonanti nazali tatu tu /m/, /n/ na /ŋ/ wakati Kihehe kina nazali nne /m/, /n/, /ŋ/ na /ŋ/.

Kihehe kina irabu kumi tu, wakati Kiingereza kinazo irabu ishirini. Orodha ya irabu za Kihehe linajumuisha irabu tano fupi ambazo kila moja inazaa irabu ndefu moja katika mazingira ya matamshi ya maneno au silabi fulani. Katika lugha ya Kihehe irabu ndefu zinabainika ikiwa utamkaji wa silabi za maneno fulani utafanyika taratibu. Jambo muhimu tulilobaini katika lugha hii ni kwamba irabu ndefu na fupi zinaweza kutumika kutofautisha maana ya neno au kubainisha maana ya neno kwa kuzingatia ngeli iliyotangulia neno lililobeba irabu husika. Hivyo basi, Kihehe kina mfumo imara wa sauti wenye jumla ya irabu kumi, ambazo ni: /ɪ/, /i:/, /e/, /ɜ:/, /a/, /a:/, /ɒ/, /ə/, /ʊ/ na /u:/ (Odden na Odden, 1999). Katika Kiingereza, irabu ishirini huanguka katika vikundi viwili. Kundi la kwanza linajumuisha irabu moja kumi na tatu; nane kati ya hizo ni fupi na tano ni irabu ndefu. Irabu moja za Kiingereza ni /ɪ/, /i:/, /e/, /ɜ:/, /a/, /a:/, /æ/, /ʌ/, /ə/, /ɒ/, /ʊ/, /u:/ na /ʊ/. Kundi la pili linajumuisha irabu-unganifu saba ambazo ni /eɪ/, /aɪ/, /ɔɪ/, /əʊ/, /aʊ/, /ɪə/, /eə/, na /ʊə/ (Roach, 2000).

Ruwaza ya Silabi na Fonotakitiki ya Kihehe

Ruwaza ya silabi ya Kihehe ni wazi, inayotawaliwa na muundo konsonanti irabu (Odden na Odden, 1999). Neno linaweza kugawanywa katika mfuatano wa vipashio vya silabi zenye kiini ambacho kinaweza kufungwa na irabu moja au irabu-unganifu inayotanguliwa au kufuatiwa na konsonanti ya pambizo isiyonekana sana inayofunikwa na konsonanti moja au kundi la konsonanti.

Muundo wa silabi wa konsonanti irabu (KI) na konsonanti irabu (KKI) hutokea zaidi kuliko miundo mingine katika Kihehe. Hata hivyo, kuna changamoto ya upangaji wa fonimu kuunda silabi katika lugha. Silabi lazima iwe na mfuatano ufuatao: silabi ya irabu moja ambayo inajumuisha irabu moja fupi pekee (I); silabi ya konsonanti irabu ambayo inajumuisha konsonanti moja na irabu moja fupi (KI); silabi ya konsonanti irabu irabu unaojumuisha konsonanti moja pamoja na irabu moja ndefu (KII); silabi ya nazali konsonanti irabu ambayo inajumuisha nazali moja, konsonanti moja pamoja na irabu moja fupi (NKI); silabi ya nazali konsonanti irabu irabu ambayo inajumuisha nazali moja, konsonanti moja pamoja na irabu moja ndefu (NKII); na silabi ya konsonanti kiyeyusho irabu ambayo inajumuisha konsonanti moja, kiyeyusho kimoja na irabu moja fupi (KYI).

Kanuni za fonotakitiki za Kiingereza huruhusu maneno kuanza na irabu, konsonanti au konsonanti na konsonanti, ambapo idadi ya juu zaidi ya konsonanti ni tatu. Katika sehemu ya mwisho, neno linaweza kuishia na irabu, konsonanti au konsonanti na konsonanti nyingine, ambapo idadi ya mfuatano isizidi konsonanti nne mfululizo (Roach, 2000). Kwa hivyo, fonotakitiki ya Kiingereza inaruhusu idadi ndogo ya ruwaza za silabi kuliko zile za Kihehe. Pamoja na hayo, Kihehe hakiruhusu neno au silabi kuanza kwa irabu ndefu, wakati katika Kiingereza, maneno na silabi huweza kuanza na irabu ndefu. Kwa hivyo, tofauti za kifonolojia kati ya Kiingereza na Kihehe hufanya maneno ya mkopo yanayoingia katika Kihehe kuwa na changamoto ya kutamkika kwa wazungumzaji wa kawaida hadi yanaposilimishwa au kuhamishwa yafungamanishwe na mfumo wa Kihehe. Katika mchakato huo kuna maneno ya mkopo huingia moja kwa moja na vipengele vyake vya kiisimu. Maneno hayo hupenyeza vipengele hivyo vya kiisimu kupitia mchakato wa usilimishaji na uhawilishaji. Michakato hiyo inaelezwa sehemu ifuatayo namna inavyoathiri fonolojia ya Kihehe kupitia maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza.

Usilimishaji wa Vipengele vya Mkopo vya Kifonolojia katika Lugha ya Kihehe

Usilimishaji ni mchakato unaorekebisha vipengele vya kiisimu vya neno la mkopo ili likubalike na mfumo wa sauti wa lugha pokezi. Katika Kihehe, mchakato wa usilimishaji unaonekana kuhusisha urekebishaji wa fonimu za neno la mkopo, muundo wa silabi na kanuni za fonotakitiki. Mchakato huo unazihusu fonimu konsonanti na irabu za mkopo kutoka lugha za kigeni ikiwamo Kiingereza. Data inaonesha fonimu konsonanti /z/, /ʃ/, /r/, /dʒ/, /v/, /ndʒ/, /ŋ/ zinazojitokeza katika maneno ya mkopo ya Kiingereza zinasilimishwa na kutamkwa kwa namna nyingine inayoendana na fonotakitiki ya lugha ya Kihehe. Uchunguzi wetu umebaini kuwa, konsonanti ya mkopo inayoingia katika Kihehe na maneno ya mkopo husilimishwa kupitia mchakato wa ubadilishaji, uhafifishaji na uingizaji. Ubadilishaji unahusisha kuweka konsonanti za mkopo na maneno ya mkopo sambamba na konsonanti za lugha pokezi ili kurahisisha matamshi. Ubadilishaji wa maneno ya mkopo ya Kiingereza katika Kihehe unahuhusisha kubadili konsonanti za Kiingereza ambazo hazitokei katika Kihehe na konsonanti nyingine za karibu zaidi na hizo zinazopatikana katika Kihehe, kama inavyooneshwaa katika (2) hapa chini.

(2) Konsonanti za Kiingereza

/ʃ/
/r/
/ŋ/

Konsonanti za Kihehe Mfano

/s/	si:lingi ‘shilling’	mammamm‘machine’
/l/	loli‘lorry’,	le:ki ‘rake’
/ŋ/	bu:kingi‘booking’,	finisingi ‘finishing’

Ingawa konsonanti /n/ inapatikana katika Kihehe, maneno ya mkopo ambayo yana sauti hiyo mwishoni ni magumu kutamkika kwa wazungumzaji wake. Kama inavyoonesha katika mifano (2), ubadilishaji wa konsonanti /r/ unahusisha kutambulisha sauti inayofanana katika mahali na namna ya utamkwaji huku ubadilishaji wa konsonanti /ʃ/ na /ŋ/ ukibusisha konsonanti za mahali tofauti pa matamshi na namna tofauti ya utamkaji. Mchakato wa ubadilishaji huchochewa zaidi na kutokuwepo kwa baadhi ya konsonanti katika orodha ya sauti za Kihehe.

Konsonanti zingine za mkopo zilizojumuishwa katika ubadilishaji ni /dʒ/ na /ndʒ/. Uchambuzi umeonesha wazi kwamba, kwa vile maneno ya mkopo yaliyo na konsonanti /dʒ/ na /ndʒ/ ni magumu kutamka, wazungumzaji huzibadilisha na konsonanti asili /gj/ na /ns/ kama inavyooneshwaa katika (3).

(3) Konsonanti za Kiingereza	Konsonanti za Kihehe	Mfano
/dʒ/	/gj/	gyagi ‘jug’ gyela ‘jail’
/ndʒ/	/ns/	silinsi ‘syringe’ chensi‘change’

Kama ilivyo katika maneno ya mkopo yenyenye konsonanti za mkopo /r/ na /ʃ/, mfumo wa sauti wa Kihehe hauna konsonanti /dʒ/ na /ndʒ/. Hivyo katika Kihehe konsonanti /dʒ/ au /ndʒ/ nafasi yake inachukuliwa na konsonanti /gj/ na /ns/ mtawalia.

Pia, tumebaini uhaihifishaji ni mchakato unaofanyika kwenye baadhi ya konsonanti za mkopo ili kufanya maneno ya mkopo yenyenye sauti husika kukubalika na wazungumzaji wa Kihehe. Uhaihifishaji unahusu konsonanti /z/ na /v/ zinapokuwa katika maneno ya mkopo kutoka Kiingereza kama inavyoonesha katika mfano (4) hapa chini.

(4) Konsonanti za Kiingereza	Konsonanti za Kihehe	Mfano
/z/	/s/	isipu ‘zip’, musiki ‘music’
/v/	/f/	fideo ‘video’ falufu‘valve’

Katika mfano (5), konsonanti ambayo ni kikwamizi ghuna /z/, inabadiliwa na kuwa konsonanti sighuna /s/. Pia konsonanti ghuna ya mdomo meno /v/ inakuwa konsonanti si ghuna ya mdomo meno /f/. Uhaihifishaji wa konosnanti /z/ na /v/ na kutamkwa kama /s/ na /f/ mtawalia, unachochewa na mahitaji ya kifonotakitiki ya lugha ya Kihehe kimatamshi na kukosekana kwa konsonanti /z/ katika orodha ya fonimu za Kihehe.

Aidha, uhaffifishaji wa /v/ unadhihirisha ukaidi fulani wa Kihehe, kwa sababu unahusisha kubadilisha konsonanti ambayo ipo katika orodha ya fonimu zake. Hii ina maana kwamba, pamoja na kuwepo katika orodha ya fonimu za lugha ya Kihehe, baadhi ya sauti zinaweza kukataliwa kama zitafanya maneno ya mkopo kuwa magumu kutamkwa, kwa sababu ya kutokea katika nafasi tofauti na pale zinapotokea katika maneno asilia ya Kihehe. Uchunguzi unaonesha kwamba, kama ilivyo katika lugha nyingine, Kihehe kinarekebisha vipegele kadhaa vya kifonolojia katika maneno ya mkopo ili yaweze kutamkika kwa kufuata otografia ya wazungumzaji wazawa wa Kihehe.

Minkova (2013), anaeleza kuwa Mame-Kiingereza haikuwa na sauti /v/, /ð/; na /z/. Kiingereza cha sasa kina sauti hizo kwa kuwa zimebadilishwa kutoka katika sauti ya asili /θ/, na /s/. Vivyo hivyo, orodha ya Kihehe haina sauti /θ/ na /z/; kwa hivyo, huhaihifishwa katika maneno ya mkopo yenyenye sauti hizo ili ziendane na mahitaji ya kifonotakitiki ya lugha hiyo. Hata hivyo, inaonesha uhaihifishaji wa sauti hiyo ni jambo la kawaida zaidi katika matamshi ya wazee na watu wasio na elimu kuliko katika matamshi ya vijana na watu wenye elimu. Tofauti hii, kwa hakika, inamaanisha kwamba usilimishaji wa kipengele fulani cha kifonolojia unategemea pia sababu za kiisimujamii kama vile umri na kiwango cha elimu rasmi. Katika Kihehe, kwa vile konsonanti /z/ na /ð/ pia hazitokei katika orodha ya konsonanti zake, maneno ya mkopo yenyenye sauti hizo hubadilishwa kwa kujaza nafasi ya sauti hizo mbili na konsonanti /s/ ya Kihehe. Hii inaonesha upekee wa lugha, ambapo fonimu mbili /z/ na /ð/ nafasi yake inachukuliwa na fonimu /s/ katika lugha ya Kihehe.

Vilevile usilimishaji unahusisha irabu. Katika Kihehe, usilimishaji wa irabu ya neno la mkopo ni dhahiri zaidi kuliko usilimishaji wa konsonanti. Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba Kiingereza kina idadi kubwa ya irabu kuliko Kihehe. Hivyo, maneno ya mkopo yenyenye irabu hizo hushindwa kutamkwa hadi yanapobadilishwa ili kuendana na fonolojia ya Kihehe. Kupitia utaratibu huo mfumo wa fonimu irabu wa Kihehe huongezeka kwa kupokea irabu mpya kupitia taratibu mbalimbali ikiwemo inavyooneshwaa na mfano (5)

(5) Irabu za Kiingereza	Irabu za Kihehe	Mifano
/ʌ/	/a: /	ba:si ‘bus’, na:ti ‘nut’
/æ/	/a: /	ka:loti ‘carrot’, ba:ngili‘bangle’
/ə/	/a/	le:na ‘learner’, swe:ta‘sweater’

Mfano (5) unaonesha irabu /ʌ/ na /æ/ zilizokopwa pamoja na maneno ya mkopo ya Kiingereza nafasi yake inabadilishwa na irabu /a:/, lakini irabu ya mkopo /ə/ inabadilishwa na irabu /a/. Usilimishaji wa irabu hizi unachagizwa na kukosekana kwa irabu /ʌ/, /æ/ na /ə/ katika orodha ya irabu za Kihehe. Hata hivyo, kama inavyofafanuliwa katika (6), ikiwa neno la mkopo lina irabu unganifu /ɪə/ /ai//eɪ//ao//ɔɪ/, wazungumzaji wa Kihehe mara nyingi wanaisilimisha kuwa kiyeyusho /j/ au /w/ ikiwa itakuwa imetanguliwa na irabu ya mbele ya juu /i/ au irabu ya nyuma ya juu /o/.

(6) Irabu ya Kiingereza Viyeyusho vya Kihehe Mifano

/ɪə/	/j/	poleya ‘player’, igiya ‘car gear’
/ai/	/j/	tayi ‘tie’, litayili ‘car tyre’
/eɪ/	/j/	peyi ‘pay’, deyiwakaa ‘day’
/ao/	/w/	Gawuni ‘gown’ bulawusi‘blouse’
/ɔɪ/	/j/	muboyi ‘boy’

Utafiti uligundua baadhi ya irabu-unganifu za mkopo zinaendelezwa katika maneno ya mkopo kwenye lugha pokezi ya Kihehe. Kwa mfano tulibaini maneno ya mkopo yenye irabu /ea/ [ɜː], /ee/ [iː] na oo/ [uː/] kutoka Kiingereza yanaendelea kuwa na irabu ndefu /ee/ [ɜː], /ii/ [iː] na /uu/ [uː] za Kihehe mtawalia. Hili linadhihirika hasa wakati otografia ya irabu ya neno la mkopo inapoendelezwa katika Kihehe. Kipengele hiki kinabainika katika mfano (7).

(7) Irabu za Kiingereza Irabu za Kihehe Mifano

/ea/ [ɜː]	/ee/ [iː]	buleeki ‘break’ leena‘learner’, gilisi ‘greas’
/ee/ [iː]	/ii/ [iː]	gilini ‘green’ wiki‘week’, kalandini ‘canteen’
/oo/ [uː]	/uu/ [uː]	buluum ‘bloom’ guudi‘good’ buuku ‘book’

Ni wazi kwamba katika Kihehe sauti ya mkopo iliyo ndani ya neno la mkopo inarekebishwa na kuhusisha hadi viyeyusho /j/ au /w/. Kwa hivyo, ukopaji wa kileksia unachombeza lugha kubadilika kiisimu ili kumudu haja ya mawasiliano ya wazungumzaji wake. Kimsingi, hata kama usilimishaji utafanana baina ya lugha, vipengele vya kifonolojia vitatofautiana kutokana na tofauti katika orodha ya sauti baina ya lugha. Hivyo, usilimishaji fonimu na urekebishaji wa kanuni za kifonotakitiki za mkopo unachochewa na hitaji la kufanya silabi ya maneno ya mkopo ya Kiingereza kuzingatia kanuni za kifonotakitiki za Kihehe, ili maneno ya mkopo yatamkwe kwa urahisi.

Kipengele kingine cha fonolojia ya Kihehe kinachoathirika na maneno ya mkopo ni silabi. Kwa kawaida silabi za Kihehe huwa na muundo wa konsonanti na irabu (KI). Hivyo, maneno yote ya mkopo kama yaliyoorodheshwa katia mfano (8) yanapoingia katika Kihehe hufanyika urekebishaji wa silabi zake kwa kuingiza irabu katikati ya konsonanti mbili zinazofuatana ili kupata muundo wa konsonanti na irabu (KI). Mifano katika (8) inaonesha jinsi mchakato huu unavyotokea katika maneno ya mkopo.

(8) Mfuatano wa Konsonanti za Kiingereza

	Mfano
bl	bulangeti ‘blanket’
pl	pulasita ‘plaster’
st	siteseni ‘station’, sitendi ‘stand’
sk	desiki ‘desk’
tr	teleni ‘train’
dr	deleva‘driver’
br	buleki ‘brake’
gr	gilisi ‘grease’
kr	kilimu ; cream’
kl	kilabu ‘club’
sh	silingi ‘shilling’

Kutokana na mfano (8), ni wazi kwamba, ruwaza za silabi ngeni kama vile [blæŋ] katika ‘blanketi’, [pla:] na [stə] katika ‘sahani’, [steɪ] na [ʃən] katika ‘station’, [sk] katika ‘dawati’, [treɪn] katika ‘treni’, [draɪ] katika ‘dereva’, [breɪk] katika ‘breki’, [gri:] kwa ‘grease’, [kri:] kwa ‘cream’, [klʌb] katika ‘club’ na [ʃɪl] na [ɪŋ] katika ‘shilingi’ imerekebishwa kwa kuingiza irabu ili kupata maneno yanayotamkwa ‘bulangeti’, ‘pulasita’, ‘siteseni’, ‘desiki’, ‘teleni’, ‘deleva’, ‘buleki’, ‘gilisi’, ‘kilimu’, ‘kilabu’ na ‘silingi’. Kama ilivyoelezwa hapo juu, uwekaji wa irabu hufanywa ili kufanya muundo wa silabi wa maneno ya mkopo ulingane na muundo wa silabi ya Kihehe wa KI na au KKI. Katika muundo wa silabi wa KKI, mfuatano wa fonimu unaweza kuwa na nazali, konsonanti na irabu fupi au ndefu; au konsonanti, kiyeyusho na irabu fupi. Kwa hakika, kanuni hizi za silabi na fonotakitiki za Kihehe hulazimisha maneno mengi ya mkopo ya Kiingereza kurekebishwa ili yafanane na maneno ya Kihehe.

Uingizaji wa Vipengele vya Kifonolojia vya Mkopo

Katika Kihehe, baadhi ya maneno ya mkopo ya Kiingereza hayajabadilishwa, badala yake yameingizwa kama yalivyo na hivyo kuathiri fonolojia ya lugha husika. Kwa mujibu wa Campbell (1998), ukopaji wa kileksika unaweza kuhusisha kueneza vipengele vya leksimu vya lugha chanzi hadi lugha pokezi. Uingizaji wa vipengele vya kifonolojia umebainika kutofautiana kati ya wazungumzaji kutegemea umri na kiwango cha elimu ya wazungumzaji. Kiujumla inaonekana wasemaji wazee na wasio na elimu kidogo huiga maneno ya mkopo, huku vijana na wazungumzaji walioelimika huyaingiza pamoja na sifa zao za kigeni za kifonolojia. Mchakato wa uingizaji, huathiri orodha ya vipashio vya kifonolojia kwa kuingiza fonimu mpya, ruwaza ya silabi na fonotakitiki ambazo hazikuwepo katika Mame-Kihehe.

Uchambuzi umeonesha konsonanti saba za Kiingereza zimebainika kuingizwa katika orodha ya fonimu za lugha ya Kihehe pamoja na maneno ya mkopo. Konsonanti hizo ni matokeo ya usilimishaji na au uhamishaji wa moja kwa moja wa maneno ya mkopo yanayotumika katika Kihehe kutoka lugha ya Kiingereza. Mfano (9) unaonesha konsonanti hizo.

(9) Konsonanti za Kiingereza	Konsonanti za Kihehe	Mifano
/r/	/r/	toro:li ‘trolley’, risi:ti ‘receipt’
/z/	/z/	zi:pu ‘zip’, batiza ‘baptize’
/ʃ/	/ʃ/	sho: kapu ‘shock up’
/ð/	/ð/	modha ‘mother’, fadha‘father’
/θ/	/θ/	bethidei ‘birth day’
/dʒ/	/dʒ/	ja:gi ‘jug’, ba:ndeji‘bandage’
/ndʒ/	/ndʒ/ or /nj/	chenji ‘change’

Utaratibu huu wa usilimishaji na uhamishaji unahuus pia irabu zinazokuwepo katika maneno ya mkopo ya Kiingereza. Ukichunguza data katika mfano (10) inaonesha irabu za Kiingereza zinazojitokeza kama zilivyo katika maneno mbalimbali ya mkopo yaliyoingia katika Kihehe. Tazama mfano (10).

(10) Irabu za Kiingereza	Irabu za Kihehe	Mifano
/ɪə/	/ɪə/	gia ‘car gear’, polea‘player’
/aɪ/	/aɪ/	taili ‘tyre’, tai ‘tie’
/eɪ/	/eɪ/	deiwaka ‘deiwe:ka
/ao/	/ao/	gauni ‘gown’, blausi ‘blouse’

Ifahamike kuwa mfumo wa fonimu za Kihehe hauna irabu-unganifu zinazoundwa silabi moja. Matokeo yake, wakati neno lenye silabi ya irabu inayoundwa na irabu-unganifu linakopwa na Kihehe, irabu hiyo hubadilishwa kuwa kiyeyusho /j/ au /w/. Kwa hiyo, kuwepo kwa irabu hizo katika Kihehe

inaonesha kuwa ziliingizwa moja kwa moja na maneno ya mkopo. Mabadiliko yanayosababishwa na mtawanyiko wa kileksika ni makubwa zaidi katika Kihehe kwani yanahusisha konsonanti na irabu. Uingizaji wa fonimu za mkopo, kwa hakika, una athiri utambulisho wa lugha husika, kwa sababu lugha hubainishwa upekee wake na fonimu zake.

Uchunguzi wetu unaonesha Kihehe kimeathirika kwa kuwa na ruwaza mpya ya silabi na kanuni za kifonotakitiki ambazo hazikuwepo katika Mame-Kihehe. Vipengele hivi vyta kifonolojia vimethibitishwa kuwa viliingia katika lugha pamoja na maneno ya mkopo pale wazungumzaji wa Kihehe walipokutana na wazungumzaji wa Kiingereza. Mchakato huo wa ukopaji wa maneno kutoka Kiingereza umeendelea kuimarika kutokana na dhima mahsusili ya iliyotengewa lugha hiyo na mamlaka za upangaji lugha nchini Tanzania na duniani. Mfano (8) ni ushahidi wa wazi unaonesha silabi kumi mahsusili za mkopo, zinazofuata fonotakitiki ya Kihehe katika maneno mbalimbali ya mkopo. Kwa hivyo, mfuatano wa konsonanti katika maneno ya Kiingereza umekopwa moja kwa moja na Kihehe kuititia maneno ya mkopo yaliyosilimishwa au kuhamishwa kwenda lugha ya Kihehe. Utaratibu huo umeathiri fonimu za Kihehe na muundo wa silabi za Kihehe.

Pamoja na hayo, uingizaji wa vipengele vya kifonolojia unaelekeea kuwa wa kawaida katika baadhi ya lugha; kutokana na msukumo wa kijamii na kiuchumi kama vile umri, jinsia, kiwango cha elimu, na umahiri katika lugha chanzi. Kuhusiana na mabadiliko ya kiisimu ambayo lugha huweza kupitia zinapokuwa katika makutano, Thomason na Kaufman (1988) na Haspelmath (2008) wanakirii kwamba umri na kiwango cha wingilugha huweza kuathiri ukopaji wa maneno ambapo athari hizo kudhahirika katika fonolojia na semantiki ya lugha pokezi.

Kama ilivyoelezwa hapo juu, udhibiti wa maneno ya mkopo katika umilisi wa Kihehe huamuliwa na umri na kiwango cha elimu ambapo vijana na wazungumzaji wa elimu hutumia maneno ya mkopo pamoja na fonimu za mkopo, huku wazee na wazungumzaji wasio wasomi wakiyaigiza katika namna ya kutamka. Fonimu za mkopo zilizoingizwa kutoka nje zinajumuisha konsonanti sita (/θ/, /z/, /ʃ/, /r/, /dʒ/, /ndʒ/) na irabu-unganifu sita (/eɪ/, /aʊ/, /ea/, /ɪə/, /aɪ/, /rɒ/). Tofauti za vipengele vya kiisimu-jamii vinavyobainisha kukubalika kwa fonimu, kwa hakika, zinakubaliana na mapitio ya maandiko kwamba katika hali za makutano ukopaji wa lugha unaweza kuathiriwa na sababu zisizo za kiisimu kama vile umri, elimu, jinsia na tabaka la kijamii (Haspelmath, 2009).

Hitimisho

Uchambuzi wa maneno ya mkopo ya Kiingereza umetoa ushahidi uliothibitisha athari za ukopaji katika fonolojia ya Kihehe. Usilimishaji na uhamishaji wa vipengele vya kiisimu vya maneno ya mkopo ya Kiingereza umechagiza ongezeko la fonimu konsonanti /z/, /ʃ/, /r/, /ŋ/, /dʒ/, /v/, na /ndʒ/; na irabu-unganifu /ʌ/, /æ/, /ə/ na /ɪə/, /ai/, /ei/, na /au/ ambazo hazikuwepo katika orodha ya fonimu za Kihehe. Data inaonesha konsonanti hizo zinaunganishwa kwa njia tofauti na konsonanti za Kihehe. Mathalani tumeona konsonanti /ʃ/ nafasi yake inachukuliwa na konsonanti ya Kihehe /s/, konsonanti /r/ nafasi yake inachukuliwa na konsonanti ya Kihehe /l/, konsonanti /ŋ/ inaongezewa konsonanti ya ngeli /g/ na kuwa /ŋg/ inayochukua nafasi ya konsonanti /ŋ/ ya neno la mkopo. Pia matokeo yanaonesha irabu /ɪə/, /ai/, /ei/ na /au/ zilizopo katika maneno ya Kiingereza zinarekebishwa kuwa /w/ au /j/ katika maneno ya mkopo ya Kiingereza yaliyopo katika Kihehe. Vilevile data inaonesha mfuatano wa konsonanti mbili (bl, pl, st, sk, tr, dr, br, gr, kr, kl, sh) unaounda silabi katika maneno ya mkopo unarekebishwa katika Kihehe kwa kuchopeka irabu katikati yake na kuunda muundo wa silabi wa konsonanti irabu (KI) unaofuata kaida ya Kihehe kimatamshi. Hivyo, ni wazi mchakato wa usilimishaji na uhamishaji wa fonimu za maneno ya mkopo ya Kiingereza unaofanywa na wazungumzaji wa Kihehe umeleta athari chanya ya ongezeko la idadi ya fonimu na miundo ya silabi katika Kihehe.

Marejeleo

- Andersson, S., Sayeed, O., na Vaux, B. (2015). *The Phonology of Language Contact*. Oxford: Oxford University Press.

Batibo, H. M. (1996). "Loanword Clusters Nativization Rules in Tswana and Swahili: A Comparative Study". *South African Journal of African Languages*, 16 (2), 33-41.

- Blommaert, J. (2013). *Ideology and Language in Tanzania: Tilburg Papers in Culture and Studies (2nd ed)*. Babylon: Tilburg.
- Campbell, L. (1998). *Historical Linguistics: An Introduction* (2 Ed.). Massachusetts: The MIT Press.
- Coetsem, F. V. (2016). *Loan Phonology and the Two Transfer Types in Language Contact*. Dordrecht: Foris Publication.
- Crystal, D. (2003). *English as a Global Language*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Dworkin, S. N. (2012). *A History of the Spanish Lexicon: A Linguistic Perspective*. New York: Oxford University Press.
- Guthrie, M. (1948 - 71). *Comparative Bantu*. Fanbrough: Clegg International Publishers.
- Haonga, E. H. (2013). Lahaja za Khehe: Mtazamo wa Kiisimu. Tasinifu ya Umahiri. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Haspelmath, M. (2009). "Lexical Borrowing: Concepts and Issues". In M. Haspelmath, *Handbook* (uk. 35-44). Berlin: De Gruyter Mouton.
- Language of Tanzania. (2012). *Atlas ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Minkova, D. (2013). *A Historical Phonology of English*. Edinburg: Edinburg University Press.
- Odden, D. na Odden, M. (1999). "Kihehe Syllable Structure". Katika H. Harry Van Der, na N. Ritter, *The Syllable: Views and acts* (uk. 417 - 445). New York: Mouton Gruyter.
- Roach, P. (2000). *English Phonetics and Phonology: A Practical Course*. Cambridge University Press.
- Sitali-Mubanga, G. N. (2018). "Some Effects of English Loanwords Adaptation into SiLozi". *International Journal of Education*, 2018 (10), 4.
- Smith, N. (2007). Contact Phonology. Katika M. Carswell Pennington, *Phonology in Contact* (uk. 76 - 108). Basingstoke: Palgrave Macmillan.
- Swilla, I. (2000). 'Borrowing in Chindali'. Katika K. Kahigi, Y. Kihore, na M. Mous, *Languages of Tanzania* (uk. 297-307). Leiden: Research for Asian, African and American Studies.
- Thomason, S. G. (2001). *Language Contact*. Edinburg: Edinburg University Press.
- Thomason, S. G. na Kaufman, T. (1988). *Language Contact, Creolization and Genetic Linguistics*. Bekeley: University of California Press.
- Walsh, M. T. (2004). *Variability and Compounding of Affixes in Hebe Animal Names (Tanzania)* Retrieved from <http://www.academia.edu> on.
- Windford, D. (2013). *The Handbook of Language Contact*. Oxford: Blackwell Publishing Ltd.